**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**
**MUHTASARI WA KIKAO CHA MENEJIMENTI CHA DHARURA KILICHOFANYIKA OKTOBA 27, 2021 KATIKA OFISI YA MKURUGENZI MTENDAJI**

## 1.0 MAHUDHURIO YA WATAALAM

| Na. | JINA KAMILI | | CHEO/WADHIFA |
|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Veronica V. Sayore | - | Mkurugenzi Mtendaji - M/Kiti |
| | **WAJUMBE** | | |
| 1. | Bw. Thomas Chogoro | - | Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara |
| 2. | Bw. Juma I. Rahisi | - | Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji |
| 3. | Bw. Elisha Mtweve | - | Kny. Kaimu Mkuu Idara ya Ujenzi |
| 4. | Bi. Evanitha Muhandikila | - | Kny. Mkuu wa Kitengo cha Sheria |
| 5. | Bw. David Pallangyo | - | Kny. Katibu Tawala (W) |
| 6. | Bw. Innocent .S. Nangay | - | Afisa Usalama (W) |
| 7. | Bw. Melkiad P. Gaka | - | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 8. | Bw. Christopher Mnebwa | - | Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi |

## 1.1 MAHUDHURIO YA WAGENI WAALIKWA - WAJUMBE

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Bw. Azizi M. Salehe | - | Mkuu wa Shule Masanza Sekondari |
| 2. | Bw. Emmanuel G. Keema | - | Mkuu wa Shule Nyangwe Sekondari |
| 3. | Bw. Godlove S. Juma | - | Mkuu wa Shule Kishamapanda Sekondari |
| 4. | Bw. Joseph Kazimoto | - | Mkuu wa Shule Athony Mtaka Sekondari |
| 5. | Bw. Aron B. Kiunsi | - | Mkuu wa Shule Kijereshi Sekondari |
| 6. | Bw. Edward M. Petro | - | Mkuu wa Shule Nassa Sekondari |
| 7. | Bw. Kija M. Maduhu | - | Mkuu wa Shule Shigala Sekondari |
| 8. | Bw. Japhet S. Joseph | - | Mkuu wa Shule Chegeni Sekondari |
| 9. | Bw. Isaya Elias | - | Kny. Mkuu wa Shule Malili Sekondari |
| 10. | Bw. Silas M. Lameck | - | Mkuu wa Shule Kalemela Sekondari |
| 11. | Bw. Lukwaja M. Makenzi | - | Mkuu wa Shule Mwasamba Sekondari |
| 12. | Bw. John M. Magulanga | - | Mkuu wa Shule Lamadi Sekondari |
| 13. | Bw. Christom J. Manyanda | - | Mkuu wa Shule Sogesca Sekondari |
| 14. | Bw. Zakayo M. Aristariko | - | Mkuu wa Shule Ngasamo Sekondari |
| 15. | Bw. Fabian J. Sendama | - | Mkuu wa Shule Badugu Sekondari |
| 16. | Bw. Marco J. Halali | - | Mkuu wa Shule Kabita Sekondari |
| 17. | Bi. Catherine R. Malegi | - | Mkuu wa Shule Mkula Sekondari |
| 18. | Bw. Hygine A.J. Komanya | - | Mkuu wa Shule Mwamagigisi Sekondari |
| 19. | Bw. Daniel S. Malimi | - | Mkuu wa Shule Nyaluhande Sekondari |

**1.2 SEKRETARIETI:**

1. Bi. Erimina T. Mosha - Mwandishi wa Vikao
2. Bw. Ramadhan Boimanda - Mwandishi wa Vikao

**2.0 MUHT: NA. BDC/MGT/DHARURA/01/10/2021 - KUFUNGUA MKUTANO.**

Katibu aliwakaribisha wajumbe katika kikao kisha Utambulisho ulifanyika na waliweza kutambuana wa nyadhifa zao: Baada ya Utambulisho alimkaribisha Mwenyekiti afungue Mkutano, naye Mwenyekiti alisimama na kutoa ufafanuzi kuhusiana na Fedha zilizoingia kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa **TZS 1,990,000,000.00** na kuchanganua shule za Msingi wamepata mgao wa kiasi cha **TZS 100,000,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa vyumba vipya 5 vya madarasa katika shule shikizi 1 na sekondari wamepata mgao wa **TZS 1,800,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa 90 kutoka mfuko wa mpango wa maendeleo ya ustawi wa Taifa wa kupambana dhidi ya **UVIKO- 19** na kiasi cha **TZS 90,000,000** kwa ajili ya Nyumba ya Mtumishi katika zahanati ya Kiloleli kata ya Masanza katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega. Pia aliwaomba wataalam kuwa wasikivu katika kuchangia hoja zitakazowasilishwa kisha alitamka kufungua kikao saa 4:26 asubuhi.

**3.0 MUHT: NA. BDC/MGT/DHARURA/02/10/2021 KURIDHIA AGENDA.**

Mwenyekiti aliwasilisha Agenda 04 katika kikao

**AGENDA.**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuridhia Agenda
3. Kupitia na kujadili taarifa ya Ujenzi wa vyumba vya madarasa 95 kutokana na kupewa kiasi cha fedha **TZS 1,990,000,000.00** kutoka mfuko wa mpango wa maendeleo ya ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya **UVIKO- 19** katika Halmashauri ya wilaya ya Busega.
4. Kufunga Kikao.

Wajumbe waliridhia Agenda hizo kwa ajili ya majadiliano.

**4.0 MUHT: NA. BDC/MGT/DHARURA/02/10/2021 - KUPITIA NA KUJADILI TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA 95 NA NYUMBA YA MTUMISHI KATIKA ZAHANATI YA KILOLELI KUTOKANA NA KUPEWA KIASI CHA FEDHA TZS 1,990,000,000.00 KUTOKA MFUKO WA MPANGO WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO- 19 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.**

Mkurugenzi Mtendaji alifafanua kuhusiana na Ujenzi wa vyumba vya madarasa 95 na ujenzi wa nyumba ya watumishi 3 kutokana na kupokea kiasi cha Fedha **TZS 1,990,000,000.00** kutoka mfuko wa mpango wa maendeleo ya ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya **UVIKO- 19** katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega. Aliendelea kwa kusema Vyumba vya madarasa vinatakiwa kukamilika ndani ya muda wa siki 50; hivyo ushirikiano na umakini unatakiwa wa kutosha kusaidia shughuli kusudiwa kukamilika kwa wakati.

Aidha, Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa, Wilaya, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, watendaji wa Kata pamoja na Wakuu wa Shule watashiriki kusimamia ujenzi wa Vyumba hivyo kwani Fedha tayari zimeshawekwa katika akaunti za shule na zahanati husika kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa Vyumba 95 vya Madarasa Pamoja na nyumba ya watumishi hivyo ufuatiliaji wa vifa vya ujenzi uanze kufanyika mapema.

Aliendelea kwa kusema tayari mawasiliano yamekwisha fanyika na SUMAJKTkuweza kusaidia kufyatua tofali kwa shule zote na atakapopatikana mzabuni kwa ajili ya kuwasilisha saruji taarifa itawasilishwa mapema.

Alitoa Rai kwa wakuu wa Shule kufanya ufuatiliaji mapema, kuwezakujua tofali zitakazohitajika kwa ajili ya ujenzi kwa kila shule kwa kuangalia uwiano kwa kila shule.

Kisha aliwasilisha.

Wajumbe waliunga mkono hoja na kupokea taarifa na kuziridhia kwa ajili ya majadiliano.

**MJADALA.**

Mjumbe alipongeza juhudi zinazofanyika kusaidia kufanikisha kazi kushudiwa kisha aliunga mkono hoja vifaa vinunuliwe kwa pamoja ili kuweza kupatikana kwa haraka.

Mjumbe alisema kuwa suluhisho limekwisha kupatikana hivyo suala la upaytikanaji wa madawati lingejadiliwa mapema ili kuweza kupata mtu atakaye tengeneza mapema kwa ajili ya shule zote.

Mjumbe alishauri kuwa mawasiliano yakafanyike mapema na **SUMAJKT** ili watengeneze madirisha na milango.

Mjumbe alihitaji kufahamu takwimu za Shule ambazo zinamarekebisho

Mkurugenzi Mtendaji alisema maombi kuhusiana na Mabadiliko katika Shule mbalimbali yamekwisha pelekwa katika Ofisi ya Rais TAMISEMI na mrejesho utakapowasilishwa wakuu wa Shule husika watajuzwa. Alimalizia kwa kusema Shule ambazo hazina mabadiliko utekelezaji wa ujenzi wa Vyumba vya madarasa ufanyike mapema.

Mjumbe alishauri ufuatiliaji ufanyike kwa haraka na kazi ya ujenzi ifanyike usiku na mchana kuhakikisha madarasa yanakamilika kwa wakati.

Mjumbe alishauri Wathibiti Wakuu Ubora wa shule wafanye ufuatiliaji mapema katika shule mpya zitakazojengwa.

Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari alisema Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule watapita katika Shule husika kwa ajili ya kukagua kuweza kupata usajili.

Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi alisema kuhusiana na malipo ya Fedha kwa wazabuni yafanyike kwa makubaliano kulingana na Mkataba iliyowasilishwa kwani wanahitaji walipwe 50% ya malipo kabla ya Kazi.

Mjumbe alisema Miongozo inaelekeza watoe huduma kwanza ndipo malipo yafanyike.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa taratibu zinatakiwa zifuatwe na shughuli zifanyike kwa uwazi ili Sheria na taratibu zilizopangwa zisivunjwe.

Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji alisema kuwa tofali zifyatuliwe mapema na Mchanga kwa ajili ya ujenzi upelekwe katika maeneo ambayo shughuli za ujenzi zitafanyika.

Mkurugenzi Mtendaji aliongezea kwa kusema Kamati za ujenzi zitatakiwa kuundwa na kutakuwa na mtu mmoja kutoka Makao Makuu ya Halmashauri atakayesimamia. Na

kuhakikisha kila darasa linakamilika kwa **TZS 20,000,000.00** na linakuwa katika Ubora unaotakiwa.

Kaimu Katibu Tawala alishukuru Wakuu wa Shule kwa ushirikiano waliouonesha na kukubaliana na mawazo yaliyotolewa; alihimiza utekelezaji ufanyike madarasa yakamilike ndani ya muda uliokudiwa.

Mkurugenzi Mtendaji alisema kuwa kufikia Desemba 05, 2021 Madarasa yanatakiwa yawe yamekamilika na Fedha zilizotengwa zisimamiwe kwa ipasavyo.

- *Baada ya Mjadala wa muda mrefu Wajumbe kwa pamoja walikubaliana SUMAJKT apatiwe kazi kwa ajili ya kuweza kufatua tofali zitakazotunika katika ujenzi wa Vyumba 95 vya madarasa.*

**5.0 MUHT: NA. BDC/MGT/DHARURA/02/10/2021 - KUFUNGA MKUTANO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti afunge Kikao, naye Mwenyekiti alisimama na kuwashukuru wajumbe kwa michango yao mizuri ya mawazo, alihimiza ushirikiano uwepo, shughuli ifanyike kwa ufanisi kusaidia madarasa kukamilika kwa wakati. Kisha alitamka kufunga mkutano saa 11:50 Jioni.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

TAREHE 27/10/2021

| | |
|---|---|
| Veronica V. Sayore | |
| **Mwenyekiti** | **Katibu** |